


# Mbweha Na Zabibu Chachu

Brigid Simiyu

Benjamin Mitchley

Kiswahili

African Storybook.org



Hapo zamani za kale, palikuwa na Mbweha aliyekuwa na njaa. Mbweha alitembea karibu na kichaka akitafuta chakula.



Aliiona mzabibu uliojaa zabibu mbivu. Kichala cha zabibu mbivu kilining'inia.



Mbweha aliwaza, "Zabibu hizi zinaonekana tamu kweli kweli." Alirudi nyuma hatua chache ili aweze kuzirukia zile zabibu.



Zabibu zilikuwa juu sana. Mbweha alipozirukia, alianguka kwa mgongo wala hakuzifikia zile zabibu.



Mbweha aliinuka akurudi nyuma zaidi ili aweze kuzifikia zabibu. Mara hii alifika karibu zaidi, lakini akaanguka tena kwa kishindo.



Alijaribu tena na tena, lakini hakuweza kuzifikia zabibu. Alianguka mara nying hadi mgongo ukamuuma.



Hatimaye, alikata tamaa na kwenda zake.



Mbweha alijawa na majuto. Alisimama, akatazama nyuma na kuziangalia tena zile zabibu, "Zabibu hizo, hata hivyo, zinaonekana chachu." Akajiliwaza. Aliondoka akaenda zake huku akihisi njaa kulikohapo awali.

You are free to download, copy, translate or adapt this story and use the illustrations as long as you attribute in the following way: Kholeka Mabeta Author - Kholeka Mabeta
Translation - Brigid Simiyu
Illustration - Benjamin Mitchley
Language - Kiswahili
Level - First paragraphs © African Storybook Initiative 2014
Creative Commons: Attribution 3.0
Source www.africanstorybook.org